dishundi huwa hili kadhalika na bundi. Tukumbuke kwamba hakuna tatizo iwapo utasema, "huyu ni bata, likichinjwa ni zuri sana kwa chakula." Hoho ni pilipili. Hapa hoho haigeuki ikawa "hoho hili" wala hatusemi hoho baya japo tamko lake linajipa uzito na utishaji. Lakini fahamu ya kwamba twaweza kusema mabata haya, mapilipili haya, madege haya, iwapo tuna madhumuni ya kuzungumza juu ya sifa za ukubwa.

Kwa muhtasari, yafaa kukumbukwa kuwa kuna shuruti maalum ambazo zinamtaka msemaji wa Kiswahili azijue na azitumie. Watu wasijifunze sheria za lugha nyingine halafu wazigagamize katika lugha ya Kiswahili. Shuruti ni kielekezo cha lugha yo yote iwayo. Kwa nini kwingine ziheshimiwe na katika Kiswahili, zisiheshimiwe?

*Sarifa*

Hii ni fani ambayo watu waliotunga sarufi ya kigeni hawakuitumia au hawakuijua au waliona itawacheleweshea kazi zao. Hakika haiwezekani kutunga sarufi ili kuongoza lugha bila kutumia fani hii ya sarifa. Fani hii ndiyo inayojulisha uwezo wa msemaji au mwandishi juu ya neno moja au mawili na jinsi yanavyohusiana. Kwa jumla sarifa katika lugha ndicho chombo ambacho kinanyoosha usemi kwa hekima na kutambulisha asili ya kila neno na jinsi lilivyopatikana pamoja na maana kadha wa kadha kwa kufuata jinsi linavyosarifiwa. Kwa ufupi maana ya sarifa ni matumizi ya maneno katika mabadiliko ya sarufi na nahau. Kwa mfano; neno *Kuzaa*—asili yake ni *kuvyaa.* Hivyo twapata uzazi, mzaliwa, mzao, mzazi, mzalishaji, mvyausa, uvyauso, mvyele, mvyeleo, kizalia, n.k. Haya yote yamesarifika kutoka katika neno kubwa moja la asili ambalo ni *kuvyaa* au *kuzaa.* Hii ni moja tu ya fadhili za sarifa tukiacha jumla ya kazi bora za kuinyoosha lugha katika fani ya sarifa ambayo pasi hiyo sarufi zetu hazikamiliki.

## UFUNDISHAJI WA VITENDAWILI

Mazungumzo haya yalitolewa tarehe 1 Aprili, 1977 katika Semina ya Waalimu wanaofundisha Kiswahili katika Shule za Sekondari, Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani; iliyotayarishwa na Taasisi ya Elimu na kufanyika katika Shule ya Sekondari ya Forodhani, Dar es Salaam.

---

*Utangulizi*

Ndugu Mwenyekiti na Ndugu Waalimu, naomba kwanza kuwashukuru wote kwa kuniruhusu na kunipa nafasi hii ya kuongea nanyi. Nafasi ya mwalimu wa kawaida kama mimi kuongea na hadhara ya waalimu kama hii mara nyingi ni haba sana. Kwa hiyo inapotokea kwa mtu wa aina yangu, huwa anawajibika kushukuru maridhawa.

Pamoja na shukrani hizo lakini Ndugu Waalimu lazima niseme

kweli—naogopa; nina hofu. Woga wangu unatokana na suala nililoombwa nilizungumzie. Suala lenyewe linahusu ufundishaji; tena ukawa ufundishaji wa vitendawili. Sote hapa tu waalimu na kila mwalimu ni mwalimu. Hivyo kila mmoja wetu hapa ana ujuzi na mbinu zake za jinsi ya kuikabili fani hii. Huu ndio woga wangu wa kwanza. Woga wangu mwingine unatokana na kutokujua kwangu kwa ukweli hasa wa hali halisi ilivyo madarasani mwetu. Mimi kwa muda wa mwaka mmoja sasa sipo katika darasa la kweli—darasa lenye uhai. Hivyo nitakachokisema hapa ni ule ujuzi wangu wa miaka miwili ya kuwa na darasa tangu tulipoanza kuifundisha rasmi Fasihi—Simulizi kama somo. Pengine inawezekana sasa mambo yamebadilika. Wenzangu wengi hapa bado mpo madarasani. Nyinyi naamini mnaifahamu na kuijua hali halisi ilivyo sasa.

Kwa hiyo Ndugu Mwenyekiti, ninachokusudia kukifanya ni kuanzisha majadiliano tu. Katika majadiliano hayo sote tuwe waalimu na wanafunzi. Tujifunze na kufundishana. Tubadilishane ujuzi na matatizo tuliyonayo katika kuikabili fani hii madarasani. Elimu haina mwisho. Na elimu ni ujuzi!

### 1. *Lengo la Fasihi*

Ndugu Mwenyekiti na Ndugu Waalimu, sote hapa baada ya kuifundisha Fasihi—Andishi ya Kiswahili kwa muda wa miaka saba sasa na Fasihi—Simulizi ya Kiswahili kwa muda wa miaka mitatu sasa, tumekwisha ona na kudhihirisha kwamba Fasihi yo yote ile *humhusu binadamu.* Hivyo lengo la Fasihi iwe ni ya maandishi au ya masimulizi ni binadamu. Binadamu anaweza katika maandishi au masimulizi yake kutumia vitu kama mimea, wanyama, mawe n.k.; lakini hatima ya yote katika kuitafakari *maana* ni lazima tuvihusishe vitu hivyo na *binadamu.* Vitu hivyo ni mifano tu. Kwa hiyo Ndugu Waalimu, tukishakubaliana na nadharia hii ya jumla, tutakuwa pia tumekwisha sema na kukubali kwamba hata vitendawili navyo (ambavyo ni fani mojawapo ya Fasihi—Simulizi) vyamhusu binadamu.

### 2. *Ukusanyaji wa Vitendawili*

(i) Ndugu Waalimu, mimi mazoea yangu ya kuvifundisha vitendawili katika vidato vya kwanza na vya pili, nilikuwa kwanza nikianza na kazi ya ukusanyaji. Kuna mbinu na mbinu za jinsi ya kukusanya vitendawili, lakini muhimu ni kwamba vitendawili ni lazima viwepo kwa matumizi ya darasa.

(a) Ukusanyaji unaweza kwa mfano ukafanyika darasani. Kila mwanafunzi anaweza akaombwa aandike vitendawili kadhaa ambavyo ataviandikia maelezo ya asili na maana. Mwalimu anaweza kuwa mratibu jumla wa kazi yote ya wanafunzi.

(b) Au pengine ukusanyaji unaweza ukafanyika darasani katika makundi. Makundi haya ya wanafunzi yanaweza kuwa ya kikabila. Hapa Ndugu Waalimu, haikusudiwi kuujenga ukabila; bali nia ni kupata mawazo ya pamoja ya wanafunzi kutokana na maeneo yao

ya maskani. Kama mbinu hii itatumika kila kundi linaweza kuratibu kazi yake.

Kazi zote katika (a) na (b) mwishoni ziletwe mbele ya darasa zima kwa majadiliano na uchambuzi kama nitakavyopendekeza baadaye.

(c) Kazi ya ukusanyaji inaweza pia ikafanyika nje ya darasa. Wanafunzi wanaweza kuruhusiwa kwa utaratibu maalum kuona na kuongea na wananchi wa eneo linaloizunguka shule. Ikumbukwe hapa Ndugu Waalimu kwamba mpango na utaratibu mzuri ni lazima uandaliwe na wananchi wanaohusika watayarishwe kabla ya wanafunzi hawajatoka nje. Kazi hii pia yaweza kufanywa na wanafunzi wakati wa likizo yao.

(ii) Inapotokea hivi itakuwa jambo zuri kama wanafunzi wataelekezwa kuandika maelezo (ingawa kwa uchache) ya watu na mazingira ya mahali ambapo vitendawili hivi vinatoka. Maelezo haya yatasaidia sana katika uchambuzi na ufafanuzi wa maana ya vitendawili.Kuhusu watu; maelezo yanaweza kwa mfano kuwa juu ya: tabia za jamii; maumbile yao; vyeo au madaraja yao, mgawanyo wao wa kazi; chakula chao, mifugo yao; mazao yao, na maisha yao kwa jumla. Kuhusu mazingira itakuwa vema kama hali ya nchi (jiografia ya mahali) itaelezwa kama ni mabonde (tambarare), milima, misitu, n.k. Ni muhimu pia kueleza vitu kama mvua, jua, kipupwe, kiangazi, n.k. vinavyoathiri maisha ya jamii inayohusika.

Baada ya wanafunzi kurudi shuleni, ningeshauri kwamba kazi ya kuratibu ifanyike darasani katika makundi ya kieneo vitendawili vilipokusanywa.

3. *Maana ya Kitendawili*

Ndugu Mwenyekiti na Ndugu Waalimu, mara nyingi mimi na madarasa yangu tumeshindwa kabisa kutoa maelezo au maana ya neno 'kitendawili' kama vile tulivyoshindwa kutoa maelezo au maana ya neno "fumbo." Kwa hali ya maneno haya yalivyo na jinsi yanavyotumiwa na Waswahili, huwa nimeridhika kufafanua neno moja kwa kutumia jingine. Hivyo nilipoulizwa kuwa "kitendawili ni nini?" Nimejibu kuwa "Kitendawili ni fumbo." Kwa hiyo hata hivi sasa Ndugu Waalimu, nafikiri kwamba kitendawili ni fumbo, tena kwa kweli ni fumbo zito sana. Fumbo nalo nafikiri ni swali lililofumbika, yaani si la moja kwa moja. Halipo wazi sana. Swali hili kwa hali na namna yo yote huhitaji akili tambuzi na pevu; akili yenye busara na hekima.

Kila tusikiapo kitendawili twafahamu kwamba lahitajika jibu. Mara nyingi ni kwamba jibu na maelezo yatolewayo ni sharti *yasadifu na kulingana na hali, tabia na mazingira ya jamii inayohusika.*

4. *Umuhimu wa Vitendawili*

(a) Ndugu Waalimu, kabla hatujajizatiti katika umuhimu wa viten-

dawili, ingefaa tukumbushane juu ya kazi na umuhimu wa taaluma ya Fasihi—Simulizi kwa jumla. Kwa ufupi Fasihi—Simulizi ya jamii yo yote ile hutenda kazi kuu tatu; nazo ni *kufufua, kuhifadhi na kukuza au kuendeleza* utamaduni wa jamii inayohusika hususa kwa njia ya masimulizi. Kumbe Fasihi—Simulizi kama tuliavyokwisha ona katika mihadhara yetu ya nyuma ni chombo muhimu sana katika jamii yo yote iwayo. Ndugu Waalimu, tukishasema hivi tutakuwa pia tumekwisha sema juu ya kazi na umuhimu wa vitendawili.

(b) **Ndugu Waalimu, vitendawili licha ya kufanya kazi hizo za jumla, huwa na umuhimu wa pekee kama fani.**

(i) **Katika jamii yetu, awali ya yote vitendawili ni *kiburudisho*. Kama kiburudisho *hufurahisha na kustarehesha*. Ndio maana kwa hiyo, vitendawili hupigwa aghalabu jioni. Huu ni wakati wa baada ya saa nyingi za kazi nzito—kazi ya kutwa. Kwa hiyo kwa watoto au wakubwa vitendawili huwa ni kitu cha kusahaulisha—yaani kustarehesha akili.**

(ii) **Ndugu Waalimu, nilikuwa nimekwishasema hapo awali kuwa 'kitendawili ni fumbo zito, fumbo linalodai jawabu na jawabu lenye maana.' Fumbo lo lote liwalo *hufikirisha*. Kitendawili huwafanya mtamba na mtambiwa kutumia *akili na busara*. Ndiyo maana pengine vitendawili hujulikana kwa jina la "Chemshabongo."**

(iii) Ndugu Waalimu. vitendawili ni vito vya hekima, Hekima ya vitendawili hupatikana kote; katika swali (kitendawili chenyewe) na katika jawabu (jibu la chemshabongo. Vitendawili *hufunza, huonya, hurudi, huelekeza na hushauri*. Kwa kifupi vitendawili *huadilisha* na *huadibu*.

(iv) **Mwisho, Ndugu Waalimu, vitendawili *huielimisha* jamii. Huweza kuielimisha jamii kisiasa, kisayansi, n.k. Elimu huenda na wakati, kadhalika na vitendawili. Kwa kadri jamii inavyojiendeleza kisiasa na kisayansi ndivyo pia vitendawili vinavyozidi kuchukua mfumo mpya.**

## UCHAMBUZI NA UFAFANUZI WA VITENDAWILI

Ndugu Mwenyekiti na Ndugu Waalimu, nilikuwa nimekwisha sema hapo awali kwamba kila mwalimu ana ujuzi na mbinu zake azitumiazo katika kulikabili somo hili. Nikasema kwamba mimi nitaanzisha mjadala tu. Naamini ndivyo nilivyofanya. Na sasa naomba tena niendelee kuwachokoza waalimu wenzangu kwa kutoa mbinu nizitumiazo katika kuchambua na kufafanua vitendawili.

Baada ya darasa kukusanya vitendawili, kazi inayobaki ni kuvichambua na kuvifafanua hivyo vitendawili. Hii ndiyo kazi niseme ngumu na muhimu zaidi. Darasa ni lazima liangalie kitendawili kimoja hadi kingine. Ni wazi kwamba kama fani nyinginezo za Fasihi—Simulizi (na kwa kweli Fasihi yote kwa jumla) kila kitendawili kina maudhui (maana) na fani (sanaa).

(a) ***Fani katika Vitendawili***

Ndugu Waalimu, mimi ninapoongea juu ya fani au sanaa katika vitendawili huwa ninaongea juu ya vitu viwili hasa—navyo ni *muundo* na *lugha*.

(i) ***Muundo***

Vitendawili vyetu vingi huwa na muundo ule ule mmoja tu. Aghalabu muundo huu huwa ni ule wa *kimapokeo; yaani wa asili*. Kama sote hapa tuzijuavyo muundo huo huwa hivi:

1. Kitangulizi—(mtambaji/mtegaji)
2. Kitendawili chenyewe.
3. Jibu (jawabu)—(mtambiwa/washiriki).
4. Kichocheo—(kama lazima).

Kwa hiyo kwa kweli mtindo mzima ni wa majibizano. Kwanza mtambaji au mtegaji hutoa *kitangulizi* kwa kusema "Kitendawili!" Msikilizaji au wasikilizaji hujibu "Tega!" Wao hukaa kimya na yeye hutua na kufikiri. Kisha hutoa kitendawili chenyewe, yaani fumbo lenyewe. Mmoja katika wasikilizaji hutakiwa atoe jawabu. Kama akishindwa mwingine ye yote anaruhusiwa kutoa jawabu. Kama wote watakuwa wameshindwa, basi wanawajibika kumshawishi mtambaji atoe jawabu mwenyewe kwa kumpa "mji" yaani *kichocheo*. Namna na aina ya kichocheo hutegemea sana mahali na mahali.

(ii) ***Lugha***

Ndugu Waalimu, vitendawili vingi vya Kiswahili hutumia picha. Picha hizi hujitokeza ama katika kitendawili (fumbo) chenyewe au katika jawabu. Picha hizi aghalabu huwa ni za vitu vinavyoonekana au kueleweka katika jamii inayohusika. Huwa ni picha kali na nzito sana. Zinashawishi na zinachoma. Pengine mifano ya vitendawili nitakayotoa itadhihirisha picha hizi:

(b) ***Maudhui (maana) katika Vitendawili***

Tunapoongea juu ya vitendawili Ndugu Waalimu, huwa tunaongea juu ya maana au ujumbe utolewao na kitendawili kinachohusika. Ujumbe wa kitendawili kama ulivyo fani nyinginezo waweza kuwa ni lengo/nia au fundisho.

Ingawa vitendawili hutumiwa zaidi na watoto au wakubwa kuwapigia watoto lakini vyenyewe si vya kitoto. Nilisema hapo nyuma kuwa vitendawili ni vito vya thamani. Hiyo thamani yake ipo wapi? Thamani ya kitendawili ni maana; ujumbe utolewao na kitendawili hicho katika kuielekeza jamii. Kwa

hiyo Ndugu Waalimu, nionavyo mimi kazi kubwa ya mwalimu na darasa lake ipo katika kuvifafanua vitendawili: Kama darasa litashindwa kufanya kazi hii basi vitendawili vitaonekana vya kitoto na havina maana.

Ndugu Waalimu, katika kuonyesha jinsi mimi ninavyofafanua vitendawili, yaani jinsi ya kulichunguza umbile la ndani la kitendawili nitatumia mifano michache ya vitendawili: Mimi nitakuwa mtambaji na ninyi washiriki (hadhira). Kama mkishindwa kunipa jawabu kwa kila kitendawili fulani, basi mtanipa "mji"—na mimi nitafurahi sana!

**Kitendawili!**
**Tega!**

1. Masikini Mandilo hupigwa kila siku jioni.
   *Jibu:* Ngozi ya kulalia.
2. Nimefuata usasi nimekwenda kuta ng'ombe nyika.
   *Jibu:* Kwenda kujisaidia porini na huko ukakutana na maafa ya nyoka au mnyama mkali.
3. Nyumbani kwetu kuna papai lililoiva lakini nashindwa kulila.
   *Jibu:* Kaka hawezi kumuoa dada yake.
4. Mshale wangu umekita kwenye mnyama, nawatafuta wazee waje kunitolea.
   *Jibu:* Mvulana kuona msichana wa kuchumbia.
5. Mume mrefu, mke mfupi lakini wanashirikiana sana.
   *Jibu:* Mchi na kinu.
6. Kata fimbo nami nikate fimbo, twende tukamuue sungura.
   *Jibu:* Kula ugali.

Tuangalie ufafanuzi wa vitendawili hivi: Vipo sita na navigawa viwili viwili. Kwa maoni yangu Ndugu Waalimu, vitendawili viwili vya kwanza vyaishauri au vyaiadilisha jamii. Hivyo vyahusu maadili, vinaifunda jamii. Cha kwanza kinasisitiza juu ya umuhimu wa kutandika na kukung'uta matandiko yetu. Watoto na wakubwa ni lazima wakung'ute shuka, mikeka, magodoro, n.k., kabla ya kulala. Na kitendawili cha pili chahimiza juu ya umuhimu wa kuchimba na kutumia vyoo. Kwenda porini vibaya. Porini kubaya—hakufai. Kuna madhara mengi. Kampeni ya "Mtu ni Afya" inaweza kuzungumziwa sana hapa.

Vitendawili viwili vinavyofuata vinahusu mila na desturi za jamii (ya Kitanzania). Kile cha kwanza kinasisitiza sana juu ya undugu na utu wa mtu. Katika makabila yetu mengi ni mwiko na ni haramu kwa kaka kumuoa dada yake. Wao huwa na upendo wa kindugu. Nidhamu ni muhimu sana. Kile cha pili nacho chaonyesha umuhimu wa kushirikiana na kutegemeana kimila. Mila na desturi yamwambia mvulana kuwa endapo amemwona msichana wa kuchumbia ni sharti awaambie wazee wake juu ya haja yake hiyo. Wao kwa

upande wao wakishirikiana na wazee wa msichana ndio watakaofanya taratibu za uchumba na hatimaye kuwaoza wahusika. Hivyo mvulana au msichana hajiamulii tu mwenyewe. Mtu binafsi haishi bila ya jamii. Na huu ndio utamaduni wetu—utamaduni wa Mtanzania.

Vitendawili viwili vya mwisho vyahusiana sana na siasa yetu ya Ujamaa na Kujitegemea. Katika vitendawili vyote viwili tunaona umuhimu wa ushirikiano. Twaambiwa kwamba umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Umoja hujenga na umoja huendeleza. Umoja na ushirikiano wa kweli ndio utakaoleta maendeleo ya kweli—maendeleo ya umma.

Ndugu Waalimu, katika vitendawili hivi twaweza kuona jinsi picha zilivyotumika. Vitu kama ngozi, ng'ombe nyika, nyoka, papai (lililoiva); mshale, nyuki, kinu na mchi vinaeleweka na vinafahamika. Mara tu tuvisikiapo twapata hisia ya namna fulani. Huu ndio mchomo. Twaambiwa jambo kwa kutumia kitu maalum.

Ndugu Mwenyekiti, nimetumia muda mwingi kueleza jambo dogo sana. Hii niliyotoa ni mifano tu. Ni wajibu wa mwalimu na darasa lake kukiangalia kila kitendawili pekee. Kila kitendawili lakini ni lazima tukipeleke katika mazingira na wakati wake. Hivi ni vitu muhimu sana katika ufafanuzi wa vitendawili.

Kwa taratibu za semina yetu Ndugu Waalimu, mchokoza mjadala ndiye pia aongozaye majadiliano. Nami nafurahi kuongoza majadiliano juu ya "*Ufundishaji wa Vitendawili.*" Namwomba kila mmoja wetu achange alicho nacho. Tubadilishane ujuzi juu ya suala hili. Ndugu Mwenyekiti, sina zaidi ya kuongeza isipokuwa labda katika majadiliano. Karibuni!!!

Asanteni sana.

## FANI KATIKA SAUTI YA DHIKI

*Sauti ya Dhiki* ni kitabu kilichoandikwa na Abdilatif Abdalla na kupigwa chapa na Shirika la "Oxford University Press' mnamo mwaka wa 1973.

*'Sauti ya Dhiki'*—imekuwa pia sauti iliyowaziba kinywa wale waliojaribu kukinyanysa Kiswahili pamoja na ushairi wake kwa jumla. Ule upinzani wao juu ya udogo wa kutotosheleza kwa Kiswahili, pamoja na bughudha kwamba mashairi yake ni mapungufu ya fani, maana na yaliyomo, hakika imehizika.

Makala haya ninayoandika, hayadai haki ya uhakiki wa ujumla wa Sauti ya Dhiki. Kazi hiyo nadhani imetekelezwa kwa kiasi katika Mulika Na: 7 na Bibi M. I. Matteru, bali yamekusudiwa kumulika jambo pekee lililosheheni uzito kwenye mashairi ya Ndugu Abdilatif Abdalla, yaliyokusanywa katika kitabu cha Sauti ya Dhiki. Sana, nitajishughulisha na 'fani' yenyewe iliyotumiwa katika kuifinyanga *"Sauti ya Dhiki,"* hata ikasibu kuwa sauti ya dhiki kweli yenye kuathiri hadi msomaji, au mwanafasihi ye yote. Katika